

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA



TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida Ndugu Ester Anania Chaula, anawataarifu Wananchi wote kwamba Tarehe **27/06/2024** kutakuwa na kikao cha Baraza la Waheshimiwa Madiwani kujadili hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)

Kikao hiki kitafanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida uliopo katika Jengo Jipya la Halmashauri ya Wilaya lililopo katika Kijiji cha Mwahango, Kata ya Ilongero.

Wananchi wote mnaombwa kuhudhuria kwenye kikao hicho muhimu kinachotarajiwa kuanza rasmi saa 8:00 Mchana.

Katika Kikao hicho, Mwananchi utapata fursa ya kusikia na kujadili hoja zilizo wasilishwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) dhidi ya Halmashauri na jinsi zinavyopatiwa ufumbuzi.

Miongoni mwa wageni watakao kuwepo kwenye kikao hicho ni pamoja na Mkuu wa Mkoa Mhe. Halima Dendego na Mkuu wa Wilaya ya Singida Mhe Godwin Gondwe pamoja na Kamati za ulinzi na Usalama Mkoa na Wilaya.

Imetolewa na,
Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali,
Halmashauri ya Wilaya ya Singida.
21.06.2024